

**Mtazamo Dhidi Yetu Wenyewe  
Sehem Ya 2 – Je Nakwa?  
(Attitude Towards Ourselves Part 2 –  
Am I Growing?)**

**Na**

**Ellis P. Forsman**

**Mtazamo Dhidi Yetu Wenyewe  
Sehem Ya 2 – Je Nakwa?  
(Attitude Towards Ourselves Part 2 –  
Am I Growing?)**

**Na**

**Ellis P. Forsman**

**Okt. 6, 2011**

# Mtazamo Dhidi Yetu Sehem Ya 2 – Je Nakua?

## Luka 6:40

Mtazamo sahihi hakika ni muhim. Ni mhimu katika kukua kwa kusanyiko la mahali fulani.

Tulijifunza kuhusu mtazamo wetu dhidi ya Mungu, Yesu Kristo, injili, kanisa, na ndugu zetu; sasa tutaendeleza somo letu katika mtazamo dhidi yetu wenyewe.

Tulijifunza sehemu ya kwanza ya mtazamo dhidi yetu wenyewe – “Jichunguze mwenyewe”. Sasa, hebu na tuangalie baadhi ya mitazamo tunayohitaji dhidi/ndani yetu wenyewe – “Je Nakuwa?”

Kukua kiroho ni uchaguzi. Tunaweza kukua kama tunataka.

Somo hili ni juu ya mtazamo wetu katika “Malengo Yetu ya Kukua Kiroho.”

Nini kinapaswa kuwa malengo yetu ya kukua kiroho? Tunapaswa kujitaahidi katika nini? Kwa vipimo gani tunaweza kujua kwamba malengo yetu yametimia na kukua kiroho kumetokea? Kama katika kila hatua, kuwa na malengo na kuzipata ni muhim katika mafanikio yo yote.

Hebu tuangalie kile ambacho kukua kwetu kiroho inatakiwa kuwa.

## Malengo ya Kinidhamu

Malengo yetu thabiti ni kuwa kama Kristo. Mwanafunzi anapaswa kuwa kama mwalimu wake. Luka 6:40, *“Mwanafunzi hawi mkuu kuliko mwalimu wake, lakini kila mtu ambaye amehitimu hulingana na mwalimu wake.”*

Mapezi ya Mungu ni kwamba tubadilishwe katika sura ya Mwanaye. Rum. 8:29, *“Maana wale aliowajua tangu asili, aliwachagua tangu asili wafananishwe na mfano wa Mwana wake, ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi.”*

Mfano – uadilifu unaofanana. “Wafananishwe” inamaanisha “wabadilishwe mfumo”. Kiuadilifu, Mungu anatutaka tuwe kama Yesu.

Tunapaswa kugeuka (au kubadilika) wenyewe katika sura ya Kristo. 2 Kor. 3:18, *“Lakini sisi sote kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.”* (Mfano ule ule – uadilifu unaofanana.)

Ni muhim kwamba tutakuwa na zaidi tuwe kama Kristo. Kama tunapobadilika tunapokuwa kimwili, tunapaswa kukua tunapokuwa kiroho, pia.

Hii inajumuisha ujuzi wa Kristo. Inaanzia mtu akiwa mdogo katika Kristo. 1 Pet. 2:2, “*Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu.*”

Wakati mtu anapofanyika mwana wa Mungu kwa mara ya kwanza anakuwa hafahamu mengi – hatarajiwi kufahamu mengi. Lakini mtu huyo anatarajiwa kukuwa katika kutamani na kujifunza neno la Mungu.

Mtu ambaye amekuwa kanisani kwa muda naye anatarajiwa kuendelea kukua, na sio kukoma.

Maji yaliyotulia mtoni hayataenda na mara yataingiliwa na uchafu ya kila aina ya wadudu, mende, na hayafai kunyweka. Maji ambayo hutirirka juu ya mwamba, hataivyo, ni masafi, mazuri na kila wakati hunyweka.

Nmaisha yetu yanapaswa kuwa hivyo, pia. Tunapokumbana na miamba ya maisha haya, inasaidia kututakasa, inatufanya kuwa bora na wenye nguvu. Tunajifunza neno la Mungu ili kutusaidia kukua na inatusaidia wakati wa shida na magumu.

Tunapaswa kuwa tunasogea na siyo kukaa mahali pamoja.

Sisi, kama Wakristo waliokomaa, tunapaswa kuwasaidia wale waliowachanga kukua. Heb. 5:12-14, “*Kwa maana iwapasapo kuwa waalimu, (maana wakati mwingi umepita), mnahitaji kufundishwa na mtu mafundisho ya kwanza ya maneno ya Mungu; nanyi mmekuwa mnahitaji maziwa wala si chakula kigumu. Kwa maana kila mtu atumiaye maziwa hajui sana neno la haki, kwa kuwa ni mtoto mchanga. Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya.*”

Tusipowafundisha watajifunza wapi?

Petro ametuagiza kukua. 2 Pet. 3:18, “*Lakini kueni katika neema na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele.*”

Wakati mwingine nafikiria kwamba ingekuwa vizuri kugeuza agizo na niiambie mwili wangu kuaacha kukua wakati napata uzito mwingi.

Lakini Petro alikuwa akiongelea miili yetu ya kiroho. Na akasema kwamba ili tukue katika neema na ujuzi wa Bwana wetu. Siyo tu ujuzi wa elimu, lakini ujuzi binafsi katika kuboresha tabia.

2 Pet. 1:5-11, “*Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu katika imani nyenu tieni na wema, na katika wema wenu, maarifa, na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, , na*

*katika saburi yenu utauwa, na katika utauwa wenu, upendano wa ndugu, upendo. Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala ssi watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. Maana yeye asiye kuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani. Kwaiyo ndugu jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo.”*

Hivyo ndio tunavyokuwa, kwa kuweka tabia moja juu ya tabia nyingine iliyojengwa katika maisha yetu ya kiroho.

Kufikia malengo yetu ya kukua kiroho inahitaji changamoto. Inahitaji juhudi madhubuti. (2 Pet. 1:5-10, hapo juu). Inahitaji juhudi zilizopo. Gal. 6:7-9, “*Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa apandacho mtu ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye katika mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; baali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele. Tena tusichoke katika kutenda mema maana tutavuna kwa wakati wake tusipozimia roho.*”

Tunaendelea na juhudi zetu hata kama tukichoka. Tunapofanya zoezi kimwili, tunachoka, siyo. Lakini karidi tunavyo fanya zoezi, inakuwa rahisi.

Lakini mwanzo wa mazoezi ya kimwili tunachoka, maumivu, kukata tamaa, na kutaka kuacha. Miili yetu inatulalamikia. Paulo anasema “Tusife moyo” au “Usiache”. Alikuwa akiongelea zoezi letu la kiroho.

1 Tim. 4:7-8, “*Bali hadithi za kizee, zisizokuwa za dini, uzikatae; nawe ujizoeze kupata utauwa. Kwa maana kujizoeza kupata nguvu za mwili kwa faa kidogo, lakini utauwa hufaa kwa mambo yote; yaani unayo ahadi ya uzima wa sasa, na ya ule utakaokuwapo baadae.*”

Paulo alisema tutavuna faida kama tusipoacha.

Kulikuwa na watu wakati wa Paulo ambao walidhani alikuwa na mshutuko kidogo na kauli yake iliwachanganya. Kwa hakika Paulo alifikiri hivyo binafsi, pia, maana kilikuwa ni kitu alichokifanyia kazi (alifikanyia zoezi). Mdo. 24:16, “*Nami ninajizoeza katika neno hili niwe na dhamiri isiyo na hatia mbele za Mungu na mbele ya watu siku zote.*”

Je tunamtazamo huo ambao unapenda kufanya zoezi (kufanyia kazi) na isiwe dhahaka kwetu?

Ukuwaji hauji kwa asili; kama hatuko makini, tunaweza kurudi nyuma katika matendo yetu ya zamani na tabia. 2 Pet. 2:20-22, “*Kwa maana wale waliokuwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana*

*ingekuwa heri kwao kama wasingalijua njia ya haki, kuliko kuijua kisha kuiacha ile amri takatifu waliopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli. Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaagaa matopeni.”*

Sawa na mazoezi yetu ya kimwili, kama tukiacha kufanya mazoezi hatutakuwa imara kama tulivyokuwa. Tunatakiwa kuendelea nayo.

Ukuwaji wa kweli unahitaji kufanywa upya kwa nia na tabia. Kitu tunachofanya mara kwa mara. Rum. 12:1-2, “*Basi ndugu zangu nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza na ukamilifu.”*

Usirudishe katika dunia; au usiwe kama dunia. Vaa nia ya Kristo. Kukubaliwa na yeye ndiyo ibada yetu yenye maana.

## **Malengo yanayofanya Kazi**

Kanisa ni mwili ulio na viungo vingi.

Kila kiungo ni muhim. 1 Kor. 12:12-22, “*Maana kama vile mwili ni mmoja nao una viungo vingi, na viungo vyote vya mwili ule, navyo ni vingi, ni mwili mmoja vivyo hivyo na Kristo. Kwa maana katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, kwamba tu Wayahudi, au kwamba tu Wayunani; ikiwa tu watumwa au ikiwa tu huru; nasi sote tulinyweshwa Roho mmoja. Kwa maana mwili si kiungo kimoja, bali ni vingi. Mguu ukisema kwa kuwa mimi si mkono, mimi si wa mwili; je! Je si wa mwili kwa sababu hiyo? Na sikio likisema kwa kuwa mimi si jicho, mimi si la mwili; je! Je si la mwili kwa sababu hiyo? Kama mwili wote ukiwa jicho, ku wapi kusikia? Kama wote ni sikio ku wapi kunusa? Bali Mungu amevitia viungo kila kimoja katika mwili kama alivyotaka. Lakini kama vyote vingekuwa kiungo kimoja, mwili ungekuwa wapi? Lakini sasa viungo ni vingi, ila mwili ni mmoja. Na jicho haliwezi kuuambia mkono, sina haja na wewe; wala tena kichwa hakiwezi kuiambia miguu, ssina haja nja ninyi. Bali zaidi sana vile viungo vya mwili vidhaniwavyo kuwa ni vinyonge zaidi vyahitajiwa zaidi.”*

Kila kiungo kinafanya kazi yake. Rum. 12:3-5, “*Kwa maana kwa neema niliyopewa namwambia kila mtu aliyeko kwenu asinie makuu kuliko ilivyompasa kunai; bali awe na nia ya kiasi, kama Mungu alivyomgawia kila mtu kiasi cha imani. Kwa kuwa kama vile katika mwili mmoja tuna viungo vingi, wala viungo vyote havitendi kazi moja. Vivyo hivyo na sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo na viungo, kila mmoja kwa mwenzake.”*

Hatupaswi kumdharau mtu mwingine eti kwa sababu tunaweza kufanya kitu kizuri kuliko yeye. Bila shaka kuna vitu ambavyo mtu anaweza kufanya vizuri kuliko mimi. Sote tunatendaa kazi tofauti kaatika mwili wa Kristo. Tunafanya kazi kwa pamoja kwa umoja, kama miili yetu. Kila mshirika anapaswa kufanya sehemu yaake.

Kama viungo vya mwili tunapaswa kukua kama mwili, kila mmoja na kwa ujumla tunapaswa kutafuta na kujenga kazi zetu kipekee katika mwili wa Kristo.

Rum. 12:6-8, *“Basi kwa kuwa tuna karama zilizo mbalimbali, kwa kadiri ya neema mliyopewa; ikiwa unabii, tutoe unabii kwa kadiri ya imani; ikiwa huduma tuwemo katika huduma yetu; mwenye kufundisha katika kufundisha kwake; mwenye kuonya katika kuonya kwake; mwenye kukirimu, kwa moyo mweupe; mwenye kusimamia kwa bidii, mwenye kurehemu, kwa furaha.”*

- Kwa baadhi itakuwa kufanya kazi katika neno (kuhubiri, kufundisha).
- Kwa wengine, inajumuisha kuwahudumia wengine (kuwatembelea, kuwahudumia).
- Kwa wengi, inajumuisha karama nyingi na uwezo.

Tunapaswa kustawisha karama zetu (kazi) katika kumfanyia Mungu kazi. 1 Pet. 4:10-11, *“Kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu. Mtu akisema na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina.”*

- Wale wanaoongea, kufanya hivyo kaama maagizo ya Mungu.
- Wale wanaohudumu, kwa uwezo waliopewa na Mungu.
- Lolote tufanyalo, tunalifanya kwa ubora wa uwezo wetu.

Kushindwa kukuwa kunaleta laana, maana tuna hatia ya kupoteza akile alichotupatia Mungu. Mfano wa Talanta. Mat. 25:14-30, *“Maana ni mfano wa mtu atakaye kusafiri, aliwaita watumwa wake akaweka kwao mali zake. Akampa mmoja talanta tano, na mmoja talanta mbili, na mmoja talanta moja; kila mtu kwa kadiri ya uwezo wake; akasafiri. Mara yule aliyepokea talanta tano akaenda akafanya biashara nazo, akachuma faida talanta nyingine tano. Vile vile na yule mwenye mbili, yeye naye akachuma nyingine mbili faida. Lakini yule aliyepokea moja alikwenda akafukua chini, akaiacha fedha ya bwana wake. Baada ya siku nyingi akaja bwana wa watumwa wale, akafanya hesabu nao. Akaja yule*

*aliyepokea talanta tano, akaleta talanta nyingine tano, akisema Bwana uliweka kwangu talanta tano; tazama nyingine tano nilizopata faida. Bwana wake akamwambia, vema mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja na yule aliyepokea talanta mbili, akasema Bwana uliweka kwangu talanta mbili, tazama talanta nyingine mbili nilizopata faida. Bwana wake akamwambia vema mtumwa mwema na mwaminifu; ulikuwa mwaminifu kwa machache, nitakuweka juu ya mengi; ingia katika furaha ya bwana wako. Akaja na yule aliyepokea talanta moja, akasema Bwana nalitambua ya kuwa wewe u mtu mgumu, wavuna usipopanda, wakusanya usipotawanya; basi nikaogopa nikaenda nikaificha talanta yako katika ardhi; tazama unayo iliyo yako. Bwana wake akajibu, akamwambia, wewe mtumwa mbaya na mlegevu, ulijua ya kuwa navuna nisipopanda, nakusanya nisipotawanya; basi ilikupasa kuiweka fedha yangu kwa watoa riba; nami nikija ningalipata iliyo yangu na faida yake. Basi mnyang'anyeni talanta hiyo, mpeni yule aliye nazo talanta kumi. Kwa maana kila mwenye kitu atapewa, na kuongezewa tele; lakini asiye na kitu, hata kile alichu nacho atanyang'anywa. Na mtumwa yule asiyefaa mtupeni mbali katika giza la nje; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.”*

Usiharibu talanta yoyote ambayo Mungu amekupa.

Tunachangamoto ya kufikia malengo yetu ya kazi. Changamoto ya kuona malengo katika mwili wa Kristo.

Siyo washirika wote walio na kazi inayofanana; jiulize mwenyewe, yangu ni ipi? Je nina mapungufu ya karama, au zinahitajika tu kukuzwa? Je hakika nimepewa karama, au natumia uwezekano huo kama udhuru wa kukuza kile ambacho hakika ninaweza?

Tuna changamoto ya kufikia malengo yetu. Kwa uzito inategemea katika kushirikiana na washirika wote.

Kama hatujashirikiana katika hitaji la kukuawa kiroho, inawezekana tukaweka malengo ambayo yatastawisha ukuaji huo. Kama hatukuwi mmoja mmoja, lengo lolote halitamizwa. Kama tunatamani kukuwa, tunapaswa kukuwa kila mmoja mmoja, na kuweka malengo yetu kuruhusu hilo!

## **Hitimisho**

Ukuwaji wa Kiroho inahitaji kuweka na kupata malengo.

Tunapoweka malengo yetu Kristo atatukuzwa! Kama mwanafunzi na kama mshirika wa mwili wake tutakuwa kile anachotaka tuwe.



Kama tunataka kukuwa kiroho, basi tunahitajika kuweka na kujitahidi katika malengo ya nidhamu na utendaji kazi ambayo itatupeleka katika mwelekeo sahihi.









